KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 17, Issue 3

20th Muharram 1433

16th Dec, 2011

YALIYOMO

TAPO LA UOKOFU 1-

TAPO LA UOKOFU

Na: Sheikh Mohamed Kasim Mazrui

Amesema Mtume (SAW) "Mayahudi walitangukana matapo sabiini na moja, Manasara wakatangukana matapo Sabiini na mbili na umma huu utatangukana matapo sabiini na tatu, yote yataingia motoni isipokuwa tapo moja tu." Akaulizwa "ni lipi tapo hilo? (litakalookoka?)" akajibu "ni tapo litakaloshikamana na haya niliyoshikamana nayo mimi na Sahaba zangu."

Katika hadithi hii tukufu muna utisho mkubwa wa kumfanya kila mwenye imani ya dini kutahadhari asianguke katika hayo matapo yatakayoangamia na kujitahidi kwa kila aliwezalo aingie katika hilo tapo litakalo okoka. Kwa sababu hii Waislamu wa kweli siku zote walikuwa wakijitahidi kufuata mwendo wa mtume (SAW) na swahaba zake, Ambao huweza kujulikana kwa hadith zilizo saheeh na hakuna hata mmoja aliyewahi kujitia katika dhamana ya mtu mwengine na akakhatarisha kutia nafsi yake katika mikono ya mwenziwe, aokoke atakapookoka yeye au aangamie atakapoangamia yeye, hata kama mtu huyo ana dini kuliko yeye mara laki na lukuki.

Hapo ndipo walipoonekana watu ambao husema neno leo, kesho likamdhihirikia kuwa lile neno alilosema jana lilikuwa ni makosa, leo akasema neno ambalo lilimdhihirikia kuwa ndilo la sawa, pasi na kujali kuitwa kigeugeu au kitatange na watu. Na ndipo walipoonekana wanafunzi wakikhalifu maneno ya mashekhe wao wakasema kinyume na walichosema wao pasi na kujali kuambiwa wamewakhalifu au wamewatia ujingani mashekhe wao.

Hao ma-Imaam wakubwa wakubwa tuwasikiyao, hakuna hata mmoja aliyejiita Imaam na kuwaambia watu "nifuateni mimi " au kuwatukulia watu dhamana ya kuokoka. Bali walikuwa wakisema "wakati wowote ikiwadhihirikia hadith ambayo yapingana na maoni yangu basi fuatani hadith, na maoni yangu yapigilieni mbali na ukuta (yaani yatupilieni mbali)."

Na wengine katika wao walipokuwa wakiwaona watu wakinakili maneno yao na kuandika wayasemayo katika darasa zao, walikuwa wakiwakataza na kuwaambia "musiandike nilisemalo leo, kwani pengine kesho naweza kudhihirikiwa na mengine nikasema jengine." Na kila Twaalib ul 'Ilm ajua kuwa kuna "qawl qadiim" na "qawl jadiid" na mwenye kupitia vitabu vya wanavyuoni wakubwa wakubwa, atawakuta katika kitabu fulani wamesema vyengine na katika kitabu chengine wamesema mengine kinyume na waliyosema mbele.

TANGAZO

JISAJILI E-MAIL YAKO KWENYE MTANDAO WETU

http://www.qssea.net

KISHA BONYEZA [OK] TUKU-TUMIE KHUTBA ZA IJUMAA NA MIHADHARA MENGINE KATIKA E-MAIL YAKO.

Yote haya ni kwa sababu ya kutafuta lililowafikiana na aliyokua ameshikamana nayo Mtume (SAW) Sahaba zake watukufu ili naye aingiebkatika tapo hilo la uokofu, na aepukane na hatari ya hayo matapo mengine.

Kabla ya kuendelea mbele yafaa tueke wazi hapa kwamba khitilafu ya kuleta huo mtangukano wa matapo mbali mbali.Bali ni khitilafu ambayo husababishwa na na jitihadi za wanavyuoni katika mambo ambayo hayakutajwa au hayakuekwa wazi katika Qur'aan na Hadith, hali ambayo imeruhusiwa (bali imeamrishwa) kutumia jihadi.

Hii ndiyo hali ya mambo yalivyokua yakiendelea katika Uislamu hapo mbeleni. Baadae wakaja watu ambao badala ya kutumia Qur'aan na hadithi za Mtume (SAW) na kujipinda katika kufuata sunna yake, waliumia meno madhihabi ya ma-Imamu na kauli za wanavyuoni, na wakajipinda kufuata sunna zao, milango ya jitihadi wakaifunga na wakalazimishana watu wawafuate hao ma-Imaamu. Qur'aan tukufu na hadithi za mtume (SAW) kila mmoja akazifasiri kutilia nguvu madhihabi ya Imaamu wake. Na aliyekuwa akisikikana akisema kuwa yeye hana madhihabi au hafuati madhihabi yoyote, au akasema neno kinyume na yaliyosemwa na wanavyuoni waliomtangulia, alikuwa akinasibishwa na kufru na Ilhaad.

Kundi la watu hawa lilisababisha kuzuka kundi jengine la watu ambao waliyapa mbele maneno yawanavyuoni kuliko maneno ya Mnguna Mtume wake hata wakapatikana katika wao watu ambao wakiambiwa Mnguasema hivi, au Mtume asema hivi wao wakasema kujasiri kusema "Lakini shekhe fulani na shekhe fulani wamesema hivi!" Ikawa maneno ya mwanachuoni na huja iliyo na mizani zaidi kwao kuliko maneno ya Mnguna Mtume wake (SAW). Katika athari kubwa na mbaya sana iliyopatikana kutokana na kundi hili ni kufikilia hadi ya kutukuzwa baadhi ya mashekhe kuliko Mtume(SAW) na kutukuzwa maneno yao kuliko maneno yake. Bali wamepatikana hata ambao wametukuza maneno ya Mngupia, na mahali pa kutajwa Mwentezi Mungu akawa hutajwa shekhe fulani na shekhe fulani.

Na katika athari mbaya zilizopatikana kutokana na kundi hili ni itikadi ya choo cha atu fulani kuwa si najisi; watu fulani wakifanya maasia ya

namna yoyote Mnguhawapatilizi kwa sababu at waoni 'Royal Family'pasi na kujali kuwa kusema hivyo humkufurisha mtu. Kwani mmoja katika misingi ya uislamu ni itikadi ya kuwamba Mngu (SWT) hakuzaa kama ambavyo hakuzaliwa. Kwa hivyo hana aila '(Family)'. Na hili ni jambo lililokaririwa katika Qur'aan mahali pengi. Na ikiwa muradi wa mwenye kusema hivyo ni kuwa hao ni 'Royal Family' wa Mtume (SAW), basi Mtume (SAW) si kazi yake kumpatiliza mtu kwa makosa aliyofanya wala kumsamehe makosa yake; hivyo ni kazi iliyohusika na Mngumwenyewe peke yake kama alivyotuwekea wazi hayo katika Qur'aan na vitabu vyengine alivyoviteremsha kabla ya Qur'aan. Mwenezi Mungu atukinge na Rehma yake kabla ya kutoka baadhi yetu katika lile tapo litakalookoka-AAMEEN.

ADA ZETU KATIKA MAZISHI

Na Sheikh: Mohamed Kasim Mazrui
1st Sept, 1980 / Shawwal 1400

Mara hii tumewatagulia wasomaji wetu makala ya Al-Ustadh Al-Imaam Sheikh Al-Amin Bin Ali aliyotangaza katika 'Sahifa' yake adad 24 ya 7 Dhul Qa'dah 1349H (1929), tini ya anwani hii:-
Hapana watu walio na ada nzuri tupu wala walio na mbaya tupu lakini wabora wa watu ni ambao husikiya jema wakalifuata na wakasikiya baya wakaliwata, na wakabadili la madhara kwa ambalo lina nafuu. Na miongoni mwa watu wenye ada mbaya nyingi kuliko njema ni sisi watu wa kimvita, hata hututahayarisha wenyewe pindi tutokewapo ni wageni. Na katika jumla ya ada mbaya tuliyo nayo ni ada zetu katika mazishi. Katika mazishi yetu muna mambo matatu – nadhani hapana wayafanyayo ila sisi peke yetu.
(LA KWANZA) Ni kutoswaliya maiti. Huona watu miya na mia**** wamekwenda kuzikani, akihudhuria maiti msikitini usione amswaliyao illa watu wanne watano.
Na pengine ukaona Twalaabul-'Ilm wako nde wazungumza ***** maiti hana wa kumswaliya ndani ya msikiti. Ni ajabu si ***** ni kuwa waliofiliwa na wenye kite na maiti hawana himma zaidi ya kumswaliya maiti wao. Bali himma yao kubwa ni kushughulika na kualika khitma na ziyara na kutafuta watu wa kusoma kaburini usiku na mtana wakakhasiri mapesa ya tarka bure kwa mambo ambayo hayakupokewa kwa Mtume (SAW), la kwa kuyafanya mwenyewe, wala Swahaba zake. Wala hayamnufaishi maiti kama alivyosema Imaam wetu Shaafi'ee. Kana kwamba hatujui kuwa kukaa makaburini usiku ni makruhu na awashaye taa kaburini ni mal'uni kwa kauli yake Mtume (SAW). Hushughulikiya mambo yasiyokuwa na asli ya dini kama haya,tukakataa yaliyoamrishwa na kusisitizwa katika dini,nayo ni kumlipia maiti deni kabla ya kumswaliya; kadhlika tukawata kumswaliya na kumuombea Mungu ambayo ndiyo sunna ya Mtume(SAW) na swahaba zake na ndiyo mambo yanayomfaa maiti kwa yakini kama alivyosema Imaam wetu Shaafi'ee. Huyawata haya na kuyashika mengine ya shaka shakaambayo hapana yakini ya kumfaa maiti au kumfikiliya.
(LA PILI) Ni katika kutukuwa maiti kwenda naye kaburini. Sunna ya Mtume (SAW) katika mazishi ni watu kuwa karibu na jeneza mbele na nyuma pasi na kusongama, na kumtukuwa maiti kimya ikimya kana kwamba kila mmoja ndiye aliyefiliwa pasi na kusoma wala kuleta dhikiri wala kupiga makelele."Sallu 'ala Nnabii" au "Ashqi Nnabii", Au mfano wa hayo. Killa mmoja awe akifikiri mauti au kukumbuka kuwa pia yeye yatamfikiliya kama yalivyomfikiliya huyo mwenziwe ili kila mmoja apate kujiandaliya nayo kwa amali njema.Huwata sunna hiyo ya mtume tukawa huwenda kuzikana kana kwamba twendao mtiya arusi nyumbani kwa viteko na furaha katika mahala ambapo tumezuiliwa hata kusoma Qur'aan na kuleta tahlil. Na tukaliwata jeneza mbele tukakaa nyuma sote tupate nafasi ya kuzungumza na kusengenyana.
(LA TATU) Ni matanga. Wamesema wanazuoni "Kheri yote ni katika kuwafuata Salaf". Na "Salaf" ni Maswahaba na Taabiina, la si waliyokuja baada ya hao (kama wadhaniavyo baahi ya watu). Ada ya Salaf ilikuwa baada ya kupelekwa ndiya yake, hapana aliyekaa matanga katika wao. Na walikuzika kila mtu alikuwa akienda na walikuwa wakiona ni maasia kwa wenye kufiliwa kufanya karamu. Na kwa ujinga wetu tumeigeuza sunna hii;walilokuwa wakiliona wao ni maasia kwetu ni sunna kuu.Walikuwa hawaweki matanga majumbani licha ya misikitini kama tufanyavyo sisi, mbali ubaya wa kufanya karamu siku ya tatu ndani ya msikiti uliojengwa kwa sababu ya ibada. Tukauondolea heshima kwa kuutapakaza uchafu na kupiga makelele. Tumeshika ada hii hata imekuwa ni lazima kila afae hufanyiwa karamu ya matanga hata kwa mali ya maiti ambayo amewatia mayatima tukazidisha haramujuuya haramu juu ya haramu. Nami nawacheleya wafanyao karamu hii na wailao kuingiya katika kauli ya Mngu(SWT). "Hakika ambao hula mali ya mayatima kwa dhulma, wala moto katika matumbo yao na watakuja ngiya motoni."

SAUTI YA HAKI

Hivi alivyosema Al-Ustaadh Al-Imaam ndivyo mambo yalivyokuwa katika wakati wake. Ama kwa siku za leo yaonekana kuwa watu waswaliyao maiti misikitini si wachache kama ilivyokuwa wakati huo.
Matanga ya Misikitini yaliyokuwako nyakati hizo yalikuwa yakikaliwa ni waume, mbali ya wanawake yakaliwapo majumbani. Sasa matanga ya waume ya msikitini yameondoka, lakini takhtima ya siku ya tatu na kufanya makaramu siku hiyo ndani ya msikiti mpaka leo yakali yakiendeleya. Hata imetukiya mwaka juzi watu kupigana kwa madonge ya haluwa katika msikiti wa Shibu, ikawa ni sababu ya Imaam wa msikiti huo kuzuiliya kusifanywe tena karamu ya namna yoyote katika msikiti huo. Na kwa bakhti nzuri maoni haya yaliwapendeza maimam wa baadhi ya misikiti mengine, nao wakaanza kuzuiya.
Kama al-Ustadh al-Imaam angekuwa hai leo angeona mtindo mpya ambao ungempa kusema zaidi kuliko haya. Mtindo wenyewe ni:
a.) Khitima za wanawake majumbani –ambako baadhi yao huwa wakisoma na wengine wazungumza na kuvuta sigara, na huku kukawa kwatolewa chai watu wakinwa. Na ghalibu watukuwao sinia za chai huwa ni wasichana waliovaa kanzu za mapajani, mmojapo akitaka kumpa mtu chai huwa hawezi kuinama mbele za watu, bal humbidi atotame. Na wakati wa kutolewa hiyo chai juzuu zilizo mikononi mwa wasomaji huwa zikipigwa kwa mateke ni hao waandazi.
b.) Ma Laudspika makaburini yakimkaribisha maiti kwa Aya za Qur'an za kina, Abdul-Baasit na Husari na wasomaji wengine. Misomo ambayo hakuna ashughulikaye nayo kuisikiza na pengine zikasomwa Aya za mirathi, kama kwamba watu wataka kugawanya mali kabla ya maiti kuzikwa.
c.) Wanawake kwenda kuzikani, jambo ambalo hapa Mvita halikuwako kabisa, limekuja zuliwa juzi na jana ni mashetani wa kibinaadamu.

UPANDE WA SALAMA

Na Sheikh: Mohamed Kasim Mazrui

Amesema Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم): “Wata lililo na shaka nawe, ufanye lisilokuwa na shaka nawe.” Hivi ni kusema “daima jiweke upande wa salama.” Wasia huu wa busara umefanywa ni mategemeo ya mambo yote ya kilimwengu na msingi mkubwa katika misingi ya dini utumiwao katika ibada, sharia na mengineyo yenye ukhusiano na dini.

Ni jambo la kusikitisha sana kuona kuwa, ingawa hakuna akanushae kuwa wasiya huu wakubaliana na akili na ilimu pia, lakini ni wachache sana wafuatao. Na hao wachache waufuatao wengi, wao huufuata katika upande uliofungamana na mambo yao ya kilimwengu tu. Na katika hao wachache wa wachache waufuatao katika mambo ya kidini, huufuata katika baadhi tu ya mambo ya ibada.

KATIKA MAMBO YA KILIMWENGU:

Mtu akitaka kujiweka upande wa salama katika ulimwengu wake yataka asijiatilie kumfanya kila mtu kuwa amekamilika hafanyi makosa. Hivi si kusema kuwa mtu awadhanie wenziwe dhana mbovu; la, bali litakikanalo ni kukumbuka tu kuwa yule mwenzio ni kiumbe, na hakuna kiumbe aliekamilika. Waweza kumdhania mwenzio kuwa ni mkweli, kumbe si mkweli, waweza kumdhania ni muaminifu, kumbe si muaminifu; waweza kumdhania kuwa akupenda kumbe hakupendi nk, nk. Kwahivyo ukiwa na siri yako ambayo hutaki ijulikane ni mtu kabisa kabisa, kujiweka upande wa salama ni kujizuilia usimpe yoyote siri hiyo kabisa kabisa. Ukumbuke kwamba ikiwa wewe mwenyewe hukuweza kuidhibiti siri yako, mtu mwengine yoyote ni awla wa kutoweza kuidhibiti, hata kama ni rafiki shafiki, au muna ukhusiano wa damu na kuonekana utungu.

Ukiwa na amana yako wataka kumpa mwenzio akuhifadhie kujiweka upande wa salama, ni kufanyiana nae mkataba, au rasiti mathalan ili iwe ni ushahidi wako kuwa umeweka amana kwa mtu fulani. Kwani taraa mtu yule akaja akageuka moyo au akapitiwa ni kalamu ya Mwenyezi Mungu akaondoka duniani, karatasi ile iwe ni ushahidi wako iwapo itahitajia.

Ukiwa wewe ni dereva ukafika mahali penye “round-about” na ikiwa ni haki yako wewe kupita na mwenzio atokeae upande mwengine akupishe, kujiweka upande wa salama ni kuhakikisha kwanza kuwa yule mwenzio ameanza kufanya maandalio ya kuzuwiya gari yake na kukupisha wewe, ndipo ujiaminishe kupita, kwani kupa wengi ambao wapeleka magari hali wamelewa, na kuna mambo hawazifahamu kanuni za ndia. Na iwapo umemtokea mtu yuwataka barabara usitosheke kwa kumpigia honi licha kumdhania kuwa amekuona, kwani pengine mtu yule akawa ni kiziwi hasikii honi yako au ni kipofu haoni kijacho wala kipitacho. Na kama utafanya upelelezi kidogo utawakuta wengi kupita mabarabarani na huku wana fikra nyingi za kuwazuilia kuona au kusikia.

Katika Qur’an tukufu tumeamrishwa tukikopeshana tuandikiane na tuweke ushahidi au rahani (Aya 282 Suratul Baqarah) hili si kwa sababu ya kutoaminiana, lakini ni kwa sababu ya kutunga upande wa salama tu.

Kama una jambo muhimu wataka kulifanya, upande wa salama ni kulifanya hivi leo na hivi sasa iwapo laweza kufanyika. Kwani kuliweka mpaka kesho au wakati mwengine ni kujitia katika khatari ya kuzukiwa ni kizuwizi au mughafala usiweze tena kulifanya. Na iwapo wewe ni mtu mwenye sifa ya sahau nyingi ni muhimu zaidi kwako kutoakhirisha lolote uwezalo kulifanya sasa hivi. Kitu chochote ambacho huna hakika kuwa kitakuletea dhara au la, kujiweka upande wa salama ni kukuiepuka kitu hicho. Hii ni mifano tu ya baadhi ya mambo ya kilimwengu ambayo kila mtu humpitia na bila ya shaka kila mtu aweza kukisia juu ya haya ametukiwa na jambo ambalo hatukulitaja hapa.

KATIKA MAMBO YA KIDINI

Kila aliesoma dini kidogo ajua kua mtu akitawadha na akafanya shaka juu ya kiungo fulani kua amekiosha au hakukiosha hutakikana ajiweke upande wa salama kwa kukiosha hicho alichokifanyia shaka. Na iwapo alitia shaka kua amekamilisha mara tatu au mara mbili tu, hua ubora kwake ni kujiweka upande wa salama, atukulie kua amekiosha mara mbili atimize ya tatu.

Katika swala, iwapo mtu amefanya shaka kua amekamilisha nguzo au rakaa hutakukana ajiweke upande wa salama atukulie kuwa hakukamilisha na akamilishe. Na hapa ni lazima tupambanue baina ya “kufanya shaka” na “kutezewa ni Ibilisi”. Ibilisi mara nyingi huwatezea watu katika kukutanisha nia na kitendo, ikawa mtu atwekwa akituliwa katika kuosha uso, kila auoshavyo huona haujaosheka, au nia ya kuosha na kitendo cha kuosha bado hazijakutana. Akitoka nae hapo akenda akamsimamia katika swala, akawa kila aifungavyo haifungiki, akawa hamalizi “takbiratul Ihram” ila hua ashamtia shaka kua nia bado haijakutana na kitendo. Na akimuata hapo, akamfuata katika sura ya Faatihah akamtia shaka juu ya kupambanua harufu, kisha akenda nae hivyo hivyo mpaka kwenye “Attahiyyatu” akawa kila aitiavyo shadda “yaa” haiingii. Hata amalizapo sala ukamuona mtu jasho lampita ndia mbili na mijite yamemjaa kanwani kwa taabu iliyompata katika kupigana na nia na kuvuta harufu. Hapo ibilisi asimame kando akimteka kwa kujua yakini kua sala ya mtu yule ni buputupu, itakundwakundwa apigwe nayo mwenyewe ya uso, maana ni sala isiyokuwa na roho ya unyenyekevu wala mazingatio. Mtu yule tangu mwanzo wa sala mpaka mwisho alikuwa ameshughulishwa ni shetani, na badili ya kumtii Mwenyezi Mngu amtii shetani bila ya kujua.

Yahadithiwa kua mtu mmoja alikwenda kwa mwanachuoni akamwambia “Sheikh! Mimi nikitaka kusali hupata taabu sana. Katika udhu mara nyingi huosha kiungo kisha nikaona sijakiosha; na nikiingia katika sala hupitiwa ni mambo kama hayo, sasa wanipa shauri gani?!” Yule sheikh akamjibu bila kusita “Nakupa shauri usijali tena!” Yule mtu akashtuka kusikia jawabu hii, akamuuliza sheikh kwa mastaajabu “Nisisali tena?!” Sheikh akamjibu “Na’am. Maana mtu afanyae kitendo kisha akaona kuwa hakukifanya, huwa ni mwendawazimu, na sala ni waajib juu ya mwenye akili tu, si waajib juu ya mwenda wazimu!” (ni dhahiri kwamba mradi wa huyu Sheikh si kumuamrisha mtu yule awate sala, lakini mradi wake ilikuwa ni kumnabihisha juu ya ubaya wa wasiwasi mwingi kua mwisho wake humpelekea mtu kua na sifa za mwandawazimu ili ajitahidi kujiepusha na wasiwasi katika kutekeleza ibada).

Katika zaka ukifanya shaka kuwa umeikamilisha au hukuikamilisha, kujiweka upande wa salama ni kuikamilisha. Mali ikiwa huna hakika kua yapasa kutolewa zaka au hayapasi, jiweke upande wa salama uyatolee zaka.

Maiti ambae wewe ndie warithi wake, ikiwa huna hakika kua mwaka aliofia aliwahi kuyatolea zaka mali yake au hakuwahi, jiweke upande wa salama uyatolee zaka.

Katika saumu kama ulitia shaka kua ulifungua kabla ya jua kutwa au ulikula daku baada ya alfajiri kutepuza, jiweke upande wa salama uilipe siku hiyo.

Na katika Hijja utakapotia shaka kua umekamilisha nguzo zake na wajibati zake, jiweke upande wa salama utekeleze kile ulicho na shaka nacho iwapo chaweza kutekelezwa au ukitolee kafara ya nyama au chenginecho kifaacho kua kafara ya hicho ulichokitilia shaka.

Katika ndoa na namna zote na mu'amalati daima jitahidi kukamilisha nguzo zilizokubaliwa ni maimamu wote ili ujiweke upande wa salama. Kwa mfano ukitaka kuoana na mwanamke, ipatikane radhi yake, radhi ya walii wake iwe mbele ya mashahidi wasiopungua wawili. Kufanya hivyo utakuwa umetatuka na khitilafi zote za wanavyuoni. Na hivyohivyo katika kuuza, kununua, kueka rahani, kuajirisha nk, nk, daima jiepushe na khitilafu za wanavyuoni, ujiweke upande wa salama.

VIPENGEE

Kipengee ni kile kilango kidogo kitiwacho katika dari ya nyumba ili ikitukia dharura ya kutaka kwenda juu ya dari, kama kuvimba (kuezeka), kuzima moto na mfano wa hayo, upatikane upenyenye wa mtu kuweza kufika darini. Kwa kuwa kilango hiki hakipitiwi ila nadira sana, basi mwenye kupita siku hiyo ya dharura ghalibu hasalimiki na uchafu ulotanda hapo au mparuzo katika mwili wake au nguo zake. Na kwa sababu hii, kila mtu hutahadhari na kupita katika kilango hicho ila kwa dharura kubwa kama hizo tulizozitaja. Basi na hivyo vipengee vitafutwavyo au vitolewavyo katika hukumu za sharia, hali yake ni kama hivyo, havifai kutumiwa ila pale patumiwapo vipengee vya gari, yaani wakati wa dharura kubwa. Na dharura ni jambo ambalo mtu asipolifanya atafikiliwa ni dharura fulani katika nafsi yake, mali yake au hishima yake. Si dharura kutafuta vipengee kwa sababu ya kutunga hawaa ya nafsi yako tu (yaani: kufuata lipendalo moyo) na kutaka kustarehe.

Kila jambo au kitu kilichoharimishwa katika sharia huwa kina madhara fulani, pengine ya dhahiri na pengine ya batini. Na mwenye kupatikana ni dharura kubwa ya kufanya jambo hilo au kutumia kitu hicho hata kama hatapata dhambi kwa sababu ya ile dharura iliyoko, lakini hatasalimika na madhara yaliyomo katika jambo lile au kitu kile. Kwa mfano: Mtu alishikwa ni kiu kubwa, na akawa hana cha kupoza kiu yake isipokuwa kileo kilicho karibu yake. Sharia yamruhusu kunwa ili kuokoa maisha yake, lakini athari ya ulevi na madhara yake hatasalimika nayo yule mwenye kunwa kwa sababu ya kuruhusiwa kunwa.

Vipengee vya sharia ni miyongoni mwa yale mambo yaliyoitwa "shubuhaat" katika ile hadeeth mashuhuri na akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "... basi mwenye kujilinda na shubuhaat Amejitakasia dini yake na cheo chake, na mwenye kuingia katika shubuhaat huingia katika haramu…" Na'am amesema kweli Mtume (صلى الله عليه وسلم): daima utawakuta wale wapendao kujitolea vipengee ndio wendeleyao kuchafua dini na kujifungulia milango ya kuingilia mambo ya haramu. Ndipo hapo walipojifungulia mlango wa kuzuilia kutekeleza nguzo ya zaka wakadai kua noti hata ikawa ya shilingi milioni haipasi kutolewa zaka, kwa sababu at noti si mali bali ni karatasi tu. Wengine wakajifungulia mlango wa kujizuilia kutekeleza nguzo ya Hijja, wakadai kua gharama za hijja siku hizi zimepindukia kiasi, na kwa hivyo si lazima hata kwa mwenye uweza; na wengine wakafanya kua yatosha kwa mtu kuata wasia wa kuhijiwa baada ya kufa kwake kwa shilingi mia tano au mia sita, badili ya kukhasiri maalfu kwa maalfu kwa kwenda yeye mwenyewe katika uhai wake.

Na hawa hawa ndio waliojifungulia mlango wa kula riba pasi na kuogopa adhabu ya Mwenyezi Mngu waliotangazwa walaji riba katika Qur'an na hadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم), hata wakaambiwa "...msipowata (kula riba) basi jiandalieni kwa vita vya Mwenyezi Mngu na Mtume wake ...". Watu hawa wakadai kua ati yafaa mtu kuuza noti ya shilingi mia n.k, kwa bei atakayo, hata kama ni shilingi alfu. Na wengine wakajihalalishia riba kwa jina la bei iliyopawa jina la "bei ya uhdah". Nayo ni mtu akitaka kumpa mwenziwe kardha kwa kutakabadhi rahani ya nyumba au shamba mathalan, waandikiane kua mwenye kutaka kardha amepokea fedha hizo kua ni thamani ya milki yake (ambayo pengine thamani ya milki hiyo ni kubwa mara tatu au nne kuliko hiyo deni aliotukua) kwa sharti atakapomregezea fedha zake nae amregezee milki yake. Maana ya bei ya namna hii ni kumuezesha yule alietoa fedha zake kutumia dakhili ipatikanayo katika milki ile ambayo sharia haimruhusu kuitumia, maana ni namna katika namna za riba.

Na watu kama hawa ndio waliojifungulia mlango wa kujihalalishia zina, wakaoa mke ambae hajaatana na mumewe na wakasahau kua zina ni jambo lenye madhara kwake hata Mwenyezi Mngu ameita "uchafu na ndia mbaya" (Aya 32 Sura Banu Israil) kwa madai ya kua atu huyu mume hasali, na asie Sali hukmu yake ni hukmu ya kafiri, na kafiri hafai kumuoa mwanamke wa ki-Islamu (hali pengine huyu mwanamke pia hasali). Na kama hivi kujisahilishia kwao kufanya mambo ya shubuhaat na kupenya katika vipengee vya sharia, kumewapelekea katika kuchafua dini zao, wakajihalalishia tupu zilizo haramu juu yao na mali ambayo yatakua ni moto ndani ya matumbo yao kama alivyotahadharisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika hadeeth tuliyotangulia kuitaja.

Siku moja Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitaka kuwabainia wafuasi wake maana ya ile Aya tukufu isemayo: "Hii ndiyo ndia yangu iliyonyooka basi ifuateni wala musifuate vidia dia vingi visije vikawakengeua na hiyo ndia Yake (iliyonyooka) (Aya 108 Surat Yusuf)." Kisha akapiga mstari ulionyoka juu ya ardhi na huku akisema, "hii ndio ndia ya Mwenyezi Mngu iliyonyooka". Kisha akapiga vistari vidogo dogo pambizoni mwa huo mstari mkubwa huku akisema "na hivi ndivyo hivyo vidia mlivyokatazwa kuvifuata. Katika kila kidia pana shetani ambae hujaribu kumkengeua mtu na hiyo barabara iliyo nyoka."

Ndia hii iliyo nyoka ndiyo ile ile ambayo kila Muislamu huiomba katika sala zake tano za mtana na usiku pindi asemapo katika Sura ya Faatihah, "Ihdinassiraatal Mustaqiim (tuongoze ndia iliyonyoka), Siraatalladhina an'amta 'alayhim ... (ndia ya wale ambao uliowane'emesha ...)". Jee umepata kuwajua au kuwafikiri ni watu gani hao? Soma Aya 69 Surat an-Nisaa' utakuta wamebainishwa na kuambiwa "hawa ndio Aliowaneemesha Mwenyezi Mngu: Manabii, Masiddiqqi na Mashahidi na watu wema". Basi kumbuka ndugu yangu kuwa kila ukisoma Faatiha huwa ukiomba Mwenyezi Mngu akutie miongoni mwa mabwana hao. Basi ikiwa wewe ni mkweli katika maombi yako hayo, bila shaka wajiandalia kuwa katika hali ya kufaa kutangamana na mabwana hao. Na hapo ndipo Mwenyezi Mngu atakapokutaqabaha maombi yako uyakaririyo katika sala zako za usiku na mtana, na akutie katika kumbo hilo Insha-Allaah.